KENYA CERTIFICATE OF BASIC EDUCATION (K.C.B.E)

GREDI 10 KISWAHILI MUHULA 1

PATHWAY: S.T.E.M, SOCIAL SCIENCE, ARTS AND SPORTS

Time: Saa 2

ELIMU YA MSINGI WA UMAHIRI

LEARNER'S DETAILS

Jina: _____

Shule: _____

Namba ya Tathmini: _____. **Tarehe:** _____

Namba ya Shule: _____. **Saini**: _____.

MAELEKEZO KWA MTAHINIWA

1. Andika jina yako,jina ya shule,namba ya mtihani,tarehe na kisha weka saini.
2. Soma maswali yote **kwa makini** kabla ya kuyajibu.
3. Mtihani una sehemu mbili:
4. Jibu **maswali yote** katika sehemu zote mbili.

VIWANGO VYA KUTATHMINI

Swali .	1	2	3	4	5	6	7	8	9	10	11	12	13	14	15	16	17	18	19	20	Jumla
Alama	2	2	2	2	2	2	1	3	2	1	1	1	1	1	2	2	2	2	3	10	100
Alama ya mtahiniwa																					
Kiwango cha tathmini																					

-KISWAHILI NA FASIHI-

-003-

-Sekonda

SEHEMU A: KISWAHILI LUGHA (ALAMA 70)

Jibu maswali yote

KAZI YA 1: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Mwalimu atasoma mazungumzo yafuatayo mara MBILI. Sikiliza kwa makini kisha ujibu maswali.

Mazungumzo

Asha: Shikamoo mwalimu. Leo nimefurahi sana kwa sababu shule yetu imeanzisha klabu ya ubunifu wa kidijitali.

Mwalimu: Marahaba Asha. Hilo ni jambo zuri sana. Unadhani klabu hiyo itawanufaisha vipi wanafunzi?

Asha: Itatusaidia kujifunza matumizi ya teknolojia, kama kuhariri video, kutengeneza mawasilisho na hata kubuni programu rahisi.

Mwalimu: Ni kweli. Teknolojia ni muhimu sana katika dunia ya leo. Je, wazazi wako wamelipokeaje wazo hilo?

Asha: Wamefurahia sana. Wanasema itaniandaa kwa ajira za baadaye na kunifanya nijitegemee.

Mwalimu: Hilo ni wazo zuri. Lakini kumbuka nidhamu na matumizi bora ya muda.

Asha: Nimekuelewa mwalimu. Nitazingatia hilo.

Maswali

1. Taja mada kuu ya mazungumzo. (Alama 2)

   _____

   _____

2. Eleza faida MOJA ya klabu ya ubunifu wa kidijitali kulingana na mazungumzo. (Alama 2)
   a. _____
   b. _____
3. Mtazamo wa wazazi wa Asha ni upi? (Alama 2)
   a. _____
   b. _____
4. Taja ushauri aliotoa mwalimu. (Alama 2)

a. _____

b. _____

5. Taja kipengele kimoja cha fani kilichotumika katika mazungumzo haya. (Alama 2)

a. _____

b. _____

KAZI YA 2: KUSOMA KWA UFAHAMU

Katika jamii ya sasa, elimu imekuwa nguzo muhimu ya maendeleo ya mtu binafsi na ya taifa kwa ujumla. Kupitia elimu, vijana hupata maarifa, stadi na maadili yanayowawezesha kuelewa mazingira yao, kutatua changamoto mbalimbali na kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa. Elimu huwafungua macho wanafunzi ili waweze kutambua vipaji vyao, kuvikuza na kuvitumia kwa manufaa yao na ya jamii inayowazunguka.

Mtaala wa umilisi umeanzishwa ili kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa shuleni haizingatii kuhifadhi taarifa pekee bali inalenga kukuza uwezo wa mwanafunzi kufikiri kwa kina, kuwa mbunifu na kujitegemea. Kupitia mtaala huu, wanafunzi hufundishwa stadi za maisha, kama vile kufanya kazi kwa ushirikiano, kuwasiliana kwa ufasaha, kutumia teknolojia na kufanya maamuzi sahihi. Hali hii huwasaidia wanafunzi kujiandaa vyema kwa maisha ya baadaye na kwa soko la ajira linalobadilika kila siku.

Hata hivyo, mafanikio ya elimu hayawezi kupatikana bila ushirikiano wa karibu kati ya walimu, wazazi na jamii kwa ujumla. Walimu wanawajibika kutoa maarifa na kuwaongoza wanafunzi, wazazi wanapaswa kutoa malezi bora na kuunga mkono shughuli za kielimu, huku jamii ikitoa mazingira salama na yenye motisha kwa kujifunza. Bila mshikamano huu, hata sera bora za elimu haziwezi kuzaa matunda. Kwa hiyo, ni wajibu wa kila mwanajamii kuthamini elimu na kushiriki kikamilifu katika kuiimarisha ili kuhakikisha maendeleo endelevu ya taifa.

Maswali

6. Eleza umuhimu wa elimu kwa mujibu wa kifungu. (Alama 2)

_____

_____

7. Taja lengo kuu la mtaala wa umilisi. (Alama 1)

_____

_____

8. Ni nani wanaohitajika kushirikiana ili elimu ifanikiwe? (Alama 3)
    a. _____
    b. _____
    c. _____
9. Eleza maana ya neno *nguzo* kama lilivyotumika kwenye kifungu. (Alama 2)

_____

_____

10. Toa kichwa mwafaka cha kifungu hiki. (Alama 1)

_____

_____

11. Taja ujumbe mmoja unaopatikana katika kifungu. (Alama 1)

_____

_____

KAZI YA 3: PENGO – KIFUNGU KILICHOPASUKA

Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa neno sahihi.

Lugha ni chombo muhimu cha _____ (12) katika jamii. Kupitia lugha, watu huweza _____ (13) mawazo yao, hisia na maarifa. Bila lugha, _____ (14) yangekuwa magumu sana. Ni jukumu la kila mtu _____ (15) lugha yake ili isiangamie. Shuleni, wanafunzi hufundishwa _____ (16) lugha kwa usahihi.

KAZI YA 4: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

17. Bainisha aina ya maneno yaliyopigiwa mstari:

a) *Mwanafunzi* anasoma kwa bidii. (Alama 1)

_____

_____

b) Walimu *wanahamasisha* wanafunzi. (Alama 2)

_____

_____

18. Tunga sentensi moja kwa kutumia:

a) Nomino ya ngeli ya A-WA. (Alama 2)

_____

_____

b) Kitenzi katika wakati uliopita. (Alama 2)

_____

_____

19. Badilisha sentensi ifuatayo kutoka wakati uliopo hadi wakati ujao:

a. Mwanafunzi anasoma kwa bidii. (Alama 3)

_____

_____

20. Sahihisha makosa ya uakifishaji katika sentensi ifuatayo:

a. mwalimu alisema elimu ni muhimu sana (Alama 4)

_____

_____

KAZI

YA 5: KUSOMA KWA UFAHAMU

Kusoma vitabu ni mojawapo ya shughuli muhimu sana katika kukuza elimu na maendeleo ya mwanafunzi. Kupitia usomaji wa vitabu mbalimbali, wanafunzi hupata fursa ya kupanua upeo wa mawazo yao na kuelewa masuala tofauti yanayohusu maisha ya kila siku, historia, sayansi, teknolojia na masuala ya kijamii. Vitabu huwafungulia wanafunzi milango ya maarifa mapya ambayo huenda wasingepata kwa kusikiliza au kutazama pekee. Kadiri mwanafunzi anavyoendelea kusoma vitabu vingi, ndivyo anavyozidi kuongeza hazina ya maarifa yake na kuwa na mtazamo mpana kuhusu dunia inayomzunguka.

Zaidi ya hayo, kusoma vitabu huwasaidia wanafunzi kukuza msamiati wao na kuimarisha matumizi sahihi ya lugha. Kupitia maneno mapya wanayokutana nayo katika vitabu, wanafunzi hujifunza maana zake, matumizi yake katika sentensi na muktadha unaofaa wa kuyatumia. Hali hii huwafanya wawe na uwezo mzuri wa kujieleza kwa maandishi na kwa mazungumzo, iwe ni darasani, nyumbani au katika jamii. Mwanafunzi anayependa kusoma huonyesha ufasaha wa lugha, ujasiri wa kuzungumza na uwezo wa kupanga mawazo yake kwa mtiririko mzuri.

Aidha, kusoma vitabu huwajengea wanafunzi nidhamu ya kujifunza na tabia ya kujitegemea. Mwanafunzi anayejenga utamaduni wa kusoma huwa na uwezo wa kujifunza peke yake bila kutegemea maelezo ya mwalimu kila wakati. Hii humsaidia kukuza fikra za kina, ubunifu na uwezo wa kutatua matatizo. Vilevile, vitabu huchangia kukuza maadili mema kama uvumilivu, bidii na kuheshimu mitazamo tofauti, hasa anaposoma hadithi na maandiko yanayowasilisha uzoefu wa watu mbalimbali.

Kwa ujumla, kusoma vitabu ni nguzo muhimu ya mafanikio ya mwanafunzi kitaaluma na kimaisha. Wazazi, walimu na jamii kwa pamoja wana wajibu wa kuwahamasisha wanafunzi kusoma vitabu kwa kuweka mazingira yanayofaa kama vile maktaba, vitabu vya kuvutia na muda maalum wa kusoma. Kwa kufanya hivyo, wanafunzi wataweza kukuza upeo wa mawazo yao, kuongeza maarifa na kuwa raia wenye uwezo wa kujieleza kwa ufasaha na kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya taifa.

Maswali

For more resources, visit cbckenyahub.com for marking schemes | 0712468452

21. Kulingana na kifungu, kusoma vitabu huwasaidia wanafunzi kupata nini? (Alama 1)

_____

_____

22. Taja jambo MOJA ambalo mwanafunzi anayependa kusoma huwa nalo kulingana na kifungu. (Alama 1)

_____

_____

23. Eleza kwa ufupi jinsi kusoma vitabu kunavyosaidia kukuza msamiati wa mwanafunzi. (Alama 1)

_____

_____

24. Kwa nini mwanafunzi anayesoma vitabu mengi huwa na uwezo mzuri wa kujieleza? (Alama 1)

_____

_____

25. Eleza mchango wa vitabu katika kukuza nidhamu ya kujifunza kwa mwanafunzi. (Alama 1)

_____

_____

26. Eleza namna kusoma vitabu kunavyoweza kumsaidia mwanafunzi kujitegemea kimaisha. (Alama 2)

_____

_____

27. Unadhani ni kwa nini wazazi na walimu wanapaswa kuwahamasisha wanafunzi kusoma vitabu?
Toa hoja MBILI. (Alama 2)

i. _____

ii. _____

28. Toa maoni yako binafsi: Je, kusoma vitabu kunaweza kuchangia vipi maendeleo ya taifa? (Alama 1)

_____

_____

29. Eleza maana ya *upeo wa mawazo*. (Alama 2)

_____

_____

30. Toa neno moja lenye maana sawa na *maarifa*. (Alama 2)

For more resources, visit cbckenyahub.com for marking schemes | 0712468452

31. Tunga sentensi moja kwa kutumia neno *kujieleza*. (Alama 2)

KAZI YA 6: UANDISHI – INSHA (ALAMA 10)

Chagua MOJA kati ya maswali yafuatayo:

1. Andika insha ya **wasifu** kuhusu mtu aliyekuhimiza kielimu. (Maneno 250–300)

AU

2. Andika **barua ya kirafiki** kwa rafiki yako ukimwalika kushiriki shughuli ya kijamii shuleni.

For more resources, visit cbckenyahub.com for marking schemes | 0712468452

SEHEMU B: KISWAHILI FASIHI (ALAMA 30)

SWALI LA 1: FASIHI SIMULIZI (ALAMA 10)

1. Eleza maana ya fasihi. (Alama 2)

2. Eleza maana ya fasihi simulizi. (Alama 2)

3. Taja sifa TATU za fasihi simulizi. (Alama 3)

a)

b) _____

c) _____

4. Eleza umuhimu WA MOJA wa fasihi simulizi katika jamii. (Alama 3)

_____

_____

SWALI LA 2: HADITHI – HEKAYA NA HURAFI (ALAMA 10)

5. Tofautisha kati ya hekaya na hurafa. (Alama 4)

_____

_____

_____

_____

6. Taja sifa TATU za hekaya au hurafa. (Alama 3)

i. _____

ii. _____

iii. _____

7. Eleza umuhimu wa hadithi hizi katika jamii. (Alama 3)

i. _____

ii. _____

iii. _____

SWALI LA 3: USHAIRI (ALAMA 10)

8. Eleza maana ya ushairi. (Alama 2)

_____

_____

9. Taja sifa TATU za ushairi kama utanzu wa fasihi. (Alama 3)

i. _____

ii. _____

iii. _____

10. Tofautisha kati ya ushairi wa arudhi na ushairi huru. (Alama 3)

_____

_____

_____

11. Eleza dhima MBILI ya ushairi katika jamii. (Alama 2)

i. _____

ii. _____

For more resources, visit cbckenyahub.com for marking schemes | 0712468452

GRADE 10 INTER C1 SENIOR SCHOOLS END OF YEAR EXAMINATIONS

ELIMU MSINGI INAYOENDANA NA UMAHIRI (CBE)

TATHMINI YA SHULE ZA SEKONDARI (DARAJA LA JUU)

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA TATU– 2026

GREDI YA 10 – FASIHI YA KISWAHILI

Muda: Saa 2

TAARIFA ZA MTAHINIWA

JINA: _____ **SHULE:** _____

DARASA: _____ **NAMBARI YA MTIHANI:** _____

TAREHE: _____ **SAINI:** _____

MAELEKEZO KWA WATAHINIWA

1. Andika jina lako na taarifa zote muhimu katika nafasi ulizopewa.
2. Karatasi hii ina sehemu mbili: **A na B**.
3. Jibu maswali yote katika sehemu zote mbili.
4. Tumia lugha ya Kiswahili sanifu katika majibu yako.
5. Andika majibu yako katika nafasi ulizoachiwa.
6. Usiondoe ukurasa wowote wa karatasi hii.

KWA MATUMIZI RASMI PEKEE (MATUMIZI YA MTAHINI)

SEHEMU	SEHEMU A	SEHEMU B	ASILIMIA (%)	KUZ 1	KUZ 2	KUF1	KUF2	KUK1	KUK2	CHI1	CHI2
WIGO LA ALAMA	ALAMA 50	ALAMA 20		90–100	75–89	58–74	41–57	31–40	21–30	11–20	1–10
POINTI				POINTI 8	POINTI 7	POINTI 6	POINTI 5	POINTI 4	POINTI 3	POINTI 2	POINTI 1
JUMLA YA ALAMA ZA MWANAFUNZI											

SEHEMU A: ALAMA 30

SWALI LA 1 – FASIHI SIMULIZI (Alama 10)

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.

Hapo zamani za kale, katika sehemu yenye vilima na mabonde ya kijani kibichi, palikuwa na kijiji kilichoitwa **Mwangaza**. Kijiji hicho kilijulikana kwa mshikamano wa wanajamii, kuheshimu wazee na kuhifadhi mila na desturi zao. Kila jioni baada ya shughuli za siku kumalizika, wanakijiji walikuwa wakikusanyika chini ya mti mkubwa uliokuwa katikati ya kijiji. Wanaume, wanawake, vijana na watoto walikaa kwa utulivu huku wakisubiri wazee

neno alilolitamka. Mara kwa mara, aliwauliza wasikilizaji maswali na kuwapa nafasi ya kujibu au kurudia baadhi ya kauli zilizokuwa muhimu katika hadithi.

Siku moja, Mzee Baraka aliwasimulia vijana hadithi ya sungura mjanja aliyekuwa akiishi msituni pamoja na wanyama wengine. Sungura alikuwa mwenye akili nyingi na aliweza kufikiri haraka wakati wa matatizo. Hata hivyo, wakati mwingine alitumia ujanja wake kuwadanganya wanyama wengine ili ajinufaishe. Katika tukio moja, sungura aliwashawishi wanyama waamini kwamba kulikuwa na mnyama mkubwa aliyekuwa akija kuwashambulia. Wanyama waliingiwa na hofu na wakaanza kukimbia bila kuchunguza ukweli wa jambo hilo.

Baadaye, wanyama waligundua kwamba sungura alikuwa amewadanganya kwa sababu alitaka kupata chakula chao na kujinufaisha peke yake. Wanyama walikasirika na kumkabili. Sungura alitambua kosa lake na kuwaomba msamaha. Wazee wa wanyama walimshauri kwamba akili na busara ni zawadi zinazopaswa kutumiwa kwa manufaa ya jamii, si kwa kuwadanganya au kuwadhuru wengine.

Mzee Baraka alipomaliza kusimulia hadithi hiyo, aliwatazama vijana na kuwauliza walichojifunza. Vijana walijadili kwa pamoja na kusema kuwa mtu mwenye akili hapaswi kutumia uwezo wake vibaya. Walieleza pia kuwa ukweli, ushirikiano, uaminifu na kuheshimiana ni muhimu katika jamii. Mzee Baraka aliwapongeza na kuwaambia kwamba hadithi kama hizo zilikuwa sehemu muhimu ya urithi wa jamii yao.

Kabla ya kuondoka, mzee huyo aliwakumbusha vijana kuwa Fasihi Simulizi haipaswi kutoweka kwa sababu ya mabadiliko ya maisha na maendeleo ya teknolojia. Aliwataka wajifunze kusimulia hadithi, nyimbo, methali na vitendawili kwa vizazi vijavyo. Vijana walikubaliana na ushauri wake na kuahidi kushiriki katika kuhifadhi utamaduni wao. Tangu siku hiyo, baadhi yao walianza kukusanya na kurekodi hadithi za wazee ili zisipotee.

Maswali

(a) Taja **sifa mbili za Fasihi Simulizi** zinazojitokeza katika kifungu hiki. **(Alama 2)**

……

……

(b) Mti mkubwa uliotajwa katika kifungu umetumiwa kama mazingira ya aina gani ya uwasilishaji wa Fasihi Simulizi? **(Alama 1)**

……

……

(c) Taja **maudhui mawili** yanayojitokeza katika kifungu hiki. **(Alama 2)**

……

……

(d) Eleza **umuhimu wa wazee** katika kuhifadhi Fasihi Simulizi kwa kurejelea kifungu. **(Alama 2)**

……

……
……

SWALI LA 2 – SEMI NA MBINU ZA KIFASIHI (Alama 10)

Jibu maswali yote.

(a) Eleza maana ya istilahi zifuatazo. (Alama 4)

(i) **Tashbihi.** (Alama 1)

……
……

(ii) **Sitiari.** (Alama 1)

……
……

(iii) **Tashihisi.** (Alama 1)

……
……

(iv) **Takriri.** (Alama 1)

……
……

(b) Tambua mbinu ya kifasihi iliyotumika katika kila sentensi ifuatayo. (Alama 4)

(i) *Asha ni simba katika uwanja wa mjadala.* (Alama 1)

……
……

(ii) *Macho yake yalikuwa kama nyota angani.* (Alama 1)

……
……

(iii) *Upepo ulivuma na kuimba kwa huzuni.* (Alama 1)

For more resources, visit cbckenyahub.com for marking schemes | 0712468452

(iv) *Twende, twende, twende hadi tufike.* (Alama 1)

……

……

(c) Eleza umuhimu mmoja wa kutumia mbinu za lugha katika kazi ya kifasihi. (Alama 1)

……

……

(d) Taja sifa moja ya lugha ya kifasihi inayotofautisha lugha hiyo na lugha ya kawaida. (Alama 1)

……

……

SWALI LA 3 – UHAKIKI WA KIFASIHI (Alama 10)

Jibu maswali yote.

(a) Tofautisha kati ya *fani* na *maudhui* katika kazi ya kifasihi. (Alama 2)

……

……

(b) Taja vipengele vinne vya fani vinavyoweza kuchanganuliwa katika kazi ya kifasihi. (Alama 4)

(i) .....

(ii) .....

(iii) .....

(iv) .....

(c) Eleza umuhimu wa wahusika katika kazi ya kifasihi. (Alama 2)

……

……

(d) Kwa nini mazingira ni muhimu katika kazi ya kifasihi? (Alama 2)

For more resources, visit cbckenyahub.com for marking schemes | 0712468452

SEHEMU B: ALAMA 50

SWALI LA 4 – (Alama 10)

Soma hadithi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Juma alisimama mbele ya nyumba yao akiwa ameshika barua mkononi. Alikuwa amepokea habari ambazo alikuwa akizisubiri kwa hamu kwa muda mrefu. Baada ya kufanya mtihani wa mwisho wa shule, alikuwa ametuma maombi ya kujiunga na shule aliyokuwa akiitamani kwa miaka mingi. Sasa alikuwa amepata nafasi hiyo. Hata hivyo, badala ya kushangilia, Juma alibaki kimya huku akiitazama barua hiyo kwa makini.

Mama yake alipotoka jikoni, alimwona mwanawe akiwa amesimama uani bila kusema lolote.

“Mbona umesimama hapo kama mtu aliyepoteza njia?” mama aliuliza kwa mshangao.

Juma hakujibu mara moja. Alimkabidhi mama yake barua hiyo bila kusema neno. Mama alifungua barua na kuanza kuisoma. Alipomaliza, macho yake yalijaa machozi ya furaha.

“Mwanangu, hii ndiyo matunda ya bidii. Nakumbuka ulivyokuwa ukisoma hadi usiku na kuamka mapema kila siku. Usisahau ulipotoka wala watu waliokusaidia kufikia hapa,” alisema mama yake.

Juma akatabasamu na kumshukuru mama yake. Alikumbuka siku ambazo alikuwa akisoma chini ya mwanga hafifu baada ya umeme kukatika. Wakati mwingine alitembea umbali mrefu kwenda shuleni, lakini hakukubali changamoto hizo zimzuie kufikia malengo yake. Marafiki zake walipokuwa wakicheza, yeye alitumia muda wake mwingi kufanya mazoezi na kusoma.

“Mama, sitawaangusha. Nitafanya kila niwezalo ili nifanikishe masomo yangu,” Juma alisema kwa ujasiri.

Mama yake akamshika begani na kumtazama kwa upendo.

“Kumbuka, mwanangu, elimu ni ufunguo wa maisha. Lakini mafanikio ya kweli hayapimwi kwa alama pekee. Nidhamu, unyenyekevu na kuwaheshimu wengine ni muhimu pia.”

Juma alitikisa kichwa kukubaliana naye. Alijua kuwa nafasi aliyokuwa ameipata haikuwa mwisho wa safari yake bali mwanzo wa safari mpya. Alikuwa tayari kukabiliana na changamoto zilizokuwa mbele yake. Akiwa ameshikilia barua hiyo kifuani, aliingia nyumbani akiwa na matumaini mapya.

(a) Taja wahusika wawili wanaojitokeza katika dondoo. **(Alama 2)**

i. .....

ii. .....

(b) Eleza sifa mbili za Juma zinazojitokeza katika dondoo. **(Alama 2)**

(c) Bainisha maudhui mawili yanayojitokeza katika dondoo hili. **(Alama 2)**

i. .....

ii. .....

(d) Eleza mbinu moja ya lugha iliyotumiwa katika dondoo hili. **(Alama 1)**

……

……

(e) Eleza umuhimu wa mazungumzo katika dondoo hili. **(Alama 1)**

……

……

(f) Pendekeza kichwa mwafaka cha dondoo hili na utoe sababu moja ya jibu lako. **(Alama 2)**

Kichwa: .....

Sababu:

.....

.....

SWALI LA 5 – USHAIRI (Alama 10)

Soma shairi lifuatalo kwa makini kisha ujibu maswali yanayofuata.

Usikate tamaa, mwana,
Ukikumbana na shida,
Jitahidi kila jana,
Kesho yako iwe bora.

Njia huwa na miiba,
Safari huwa na vikwazo,
Mvumilivu hushinda,
Na mwenye bidii hufika.

Elimu ni taa njiani,
Maarifa ni nguvu yako,
Usidharau juhudi,
Maisha yatang'ara.

Unaposhindwa usilie,
Inuka uanze tena,

Kwa bidii na uvumilivu,
Utafikia malengo yako.

MASWALI

(a) Shairi hili linahusu nini? **(Alama 1)**

……
……

(b) Taja maudhui mawili yanayojitokeza katika shairi hili. **(Alama 2)**

(i) .....

(ii) .....

(c) Eleza maana ya mshororo ufuatao kama ulivyotumiwa katika shairi. **(Alama 2)**

"Elimu ni taa njiani."

……
……

(d) Taja mbinu mbili za lugha zilizotumiwa katika shairi hili. **(Alama 2)**

(i) .....

(ii) .....

(e) Eleza ujumbe unaopatikana katika shairi hili. **(Alama 2)**

……
……

(f) Taja sifa moja ya mshairi inayoweza kubainishwa kutokana na shairi hili. **(Alama 1)**

……

Soma dondoo lifuatalo kwa makini kisha ujibu maswali yanayofuata.

DINCO: Katika karne hii bado unapima uwezo wa kiongozi kwa kigezo cha jinsia? Hii ni dunia ya usasa leo, ndugu. *(Anaweka kibonzo cha sungura aliyebeba kipaza sauti na kuuliza kama kidatu kipo sawa.)*

KIZITO: Visiki vyote lazima viondolewe. Awezaye kuviangusha ni Mulika tu! Wampendaye wampenda kwa dhati na wamchukiaye nao humchukia kwa dhati. *(Anaweka kibonzo kinachofagia.)*

MBUYU: Ee bwana, siasa si chakacha, ni misuli ya kupigana na mibabe, ni kampeni za maneno matamu ya kupata kura. Huo usasa mnaozungumzia hauna msingi. Siasa si mashindano ya urembo na mavazi... *(Anaweka kibonzo kinachopiga yowe.)*

KIZITO: Wewe umepofushwa na vipeni vichache unavyotumiwa kila juma kupitia simu. Mtegemea nundu...

MBUYU: Nani kakuzuia nawe usivipate? Ukitaka kula asali, kaa na nyuki...

KIZITO: Lazima uchunguze malighafi anayoitumia nyuki kwenye sega. Nyuki wa siku hizi si nyuki asili. Ni mfano wa nyuki. Hawaaminiki. Raundi hii mawimbi ya mabadiliko yametufikia.

MBUYU: *(Anaweka vibonzo viwili vinavyocheka hadi kutoa machozi.)* Eti mabadiliko? Nguo kuukuu haiwi mpya kwa kupigwa viraka. Mulika ni adui wa maendeleo na ufanisi.

MUSA: Kwa nini umeamua kuondoka kijijini bila kuwaambia wazazi wako?

NEEMA: Niliogopa kwamba hawangenielewa.

MUSA: Lakini kukimbia tatizo hakutalimaliza.

NEEMA: Unafikiri nifanye nini basi?

MUSA: Waambie ukweli. Wazazi wanaweza kukasirika, lakini baadaye wataelewa.

NEEMA: Labda uko sahihi. Nimekuwa nikikimbia kwa sababu ya hofu.

MUSA: Ujasiri si kutokuwa na hofu. Ujasiri ni kukabiliana na hofu.

MASWALI

(a) Taja wahusika wawili wanaojitokeza katika dondoo hili. (Alama 2)

(b) Eleza sifa mbili za Musa zinazojitokeza katika dondoo. (Alama 2)

(i) .....

(ii) .....

(c) Taja maudhui mawili yanayojitokeza katika dondoo hili. (Alama 2)

(i) .....

(ii) .....

(d) Eleza umuhimu wa matumizi ya mazungumzo katika tamthilia. (Alama 2)

.....

.....

(e) Taja mbinu moja ya kisanaa inayojitokeza katika dondoo hili na ueleze jinsi ilivyotumiwa. (Alama 2)

Mbinu: .....

Maelezo:

.....

.....

SWALI LA 7 – FASIHI SIMULIZI NA JAMII (Alama 10)

Jibu maswali yote.

(a) Eleza tofauti kati ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo. (Alama 6)

(i) Uwasilishaji (Alama 2)

Fasihi Simulizi:

……

……

Fasihi Andishi:

……

Fasihi Simulizi:

……

……

Fasihi Andishi:

……

……

(iii) Hadhira (Alama 2)

Fasihi Simulizi:

……

……

Fasihi Andishi:

……

……

(b) Taja vipera vinne vya Fasihi Simulizi. (Alama 2)

(i) .....

(ii) .....

(iii) .....

(iv) .....

(c) Eleza umuhimu wa Fasihi Simulizi katika jamii ya kisasa. (Alama 2)

……

……

SWALI LA 8 – UHAKIKI WA KAZI YA KIFASIHI (Alama 10)

Jibu swali hili kwa kurejelea kazi yoyote ya kifasihi uliyosoma darasani.

Thibitisha kauli hii kwa hoja tano, ukitoa mifano mwafaka kutoka katika kazi ya kifasihi uliyosoma. (Alama 10)

(i) .....

(ii) .....

(iii) .....

(iv) .....

(v) .....

GRADE 10 INTER C1 SENIOR SCHOOLS END OF YEAR EXAMINATIONS

CHETI CHA ELIMU YA MSINGI KENYA (KCBE)
TATHMINI YA SHULE YA UPILI YA JUU
TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA WA 3, 2026
GREDI YA 10 – KISWAHILI
Muda: Saa 2

TAARIFA ZA MWANAFUNZI

Jina: _____ Shule: _____

Nambari ya Tathmini: _____ Tarehe: _____

Nambari ya Shule: _____ Sahihi: _____

MAELEKEZO KWA WANAFUNZI

1. Andika jina lako katika nafasi ulizopewa hapo juu.
2. Andika jina la shule yako na darasa lako katika nafasi ulizopewa.
3. Andika nambari yako ya usajili na tarehe ya tathmini katika nafasi ulizopewa.
4. Karatasi hii ina sehemu mbili: A na B.
5. Jibu maswali yote katika sehemu A na sehemu B.
6. Jibu maswali kwa lugha ya Kiswahili.
7. Majibu yote LAZIMA yaandikwe katika nafasi ulizopewa kwenye karatasi hii.
8. USIONDOE ukurasa wowote kutoka kwenye karatasi hii ya maswali.

ALAMA ZA MWANAFUNZI

SEHEMU	SEHEMU A	SEHEMU B	ASILIMIA (%)	KUZ 1	KUZ 2	KUF 1	KUF 2	KUK 1	KUK 2	CHI 1	CHI12
KIWANGO CHA ALAMA	ALAMA 30	ALAMA 50		90-100	75-89	58-74	41-57	31-40	21-30	11-20	1-10
POINTI			8 POINTI	7 POINTI	6 POINTI	5 POINTI	4 POINTI	3 POINTI	2 POINTI	1 POINTI	
JUMLA YA ALAMA ZA MWANAFUNZI											

SEHEMU A: ALAMA 50

KAZI YA 1: UFAHAMU Alama 10

1. **Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Teknolojia imekuwa sehemu muhimu ya maisha ya binadamu katika karne ya ishirini na moja. Katika sekta ya elimu, matumizi ya vifaa vya kidijitali yamebadilisha namna wanafunzi wanavyopata na

darasani. Leo hii, mwanafunzi anaweza kupata taarifa kutoka kwenye maktaba za kidijitali, tovuti za kielimu, video na programu mbalimbali za kujifunzia.

Matumizi ya teknolojia shuleni yana manufaa mengi. Kwanza, humwezesha mwanafunzi kupata taarifa kwa haraka. Pili, huleta mazingira ya kujifunza yenye kuvutia kwa kutumia picha, sauti, video na michoro. Tatu, teknolojia huwawezesha wanafunzi kushirikiana katika miradi hata kama hawako sehemu moja. Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kutumia majukwaa ya mtandao kufanya utafiti na kuandaa kazi za pamoja.

Hata hivyo, teknolojia inapaswa kutumiwa kwa uwajibikaji. Baadhi ya wanafunzi hutumia vifaa vya kidijitali kwa shughuli zisizohusiana na masomo. Wengine huamini kila taarifa wanayopata kwenye mtandao bila kuichunguza. Hali hii inaweza kusababisha upotoshaji wa taarifa. Kwa hiyo, mwanafunzi anapaswa kuwa na uwezo wa kutathmini chanzo cha taarifa kabla ya kuitumia.

Walimu na wazazi pia wana jukumu la kuwaongoza vijana katika matumizi salama ya teknolojia. Wanafunzi wanapaswa kufundishwa namna ya kulinda taarifa zao binafsi, kuheshimu haki za wengine na kutumia mitandao kwa mawasiliano yenye kujenga. Teknolojia ikitumiwa vizuri, inaweza kuwa chombo muhimu cha kukuza ubunifu, utafiti na maendeleo ya kielimu.

Maswali

a) Taja **manufaa mawili** ya teknolojia katika elimu yaliyotajwa katika kifungu. **(2 alama)**

_____

_____

b) Eleza kwa nini mwanafunzi hapaswi kuamini kila taarifa anayopata kwenye mtandao. **(2 alama)**

_____

_____

c) Taja njia **mbili** ambazo wanafunzi wanaweza kutumia teknolojia kushirikiana katika masomo. **(2 alama)**

_____

_____

_____

_____

e) Pendekeza njia mbili ambazo mwanafunzi anaweza kutumia ili kuwa mtumiaji mwajibikaji wa teknolojia. **(2 alama)**

_____

_____

KAZI YA 2: Alama 10

2. Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa neno linalofaa ili kukamilisha kifungu hiki.

UHIFADHI WA MAZINGIRA

Mazingira ni sehemu muhimu ya maisha ya binadamu. Kila mtu ana wajibu wa _____ (a) mazingira yake ili yaendelee kuwa safi na salama. Misitu hutupatia hewa safi na husaidia _____ (b) mmomonyoko wa udongo. Kwa sababu hiyo, ni muhimu kupanda _____ (c) na kuzuia ukataji wa miti kiholela.

Katika jamii nyingi, taka zimekuwa _____ (d) kubwa la kimazingira. Taka zisiposimamiwa vizuri zinaweza _____ (e) mazingira na kusababisha magonjwa. Wananchi wanapaswa kutenganisha taka zinazoweza _____ (f) kutoka kwa zile zisizoweza kutumika tena.

Shule pia zina nafasi muhimu katika uhifadhi wa mazingira. Wanafunzi wanaweza kuanzisha miradi ya _____ (g) miti, kusafisha mazingira na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa mazingira. Aidha, maji yanapaswa kutumiwa kwa _____ (h) ili kuzuia upotevu wake.

Ni wajibu wa kila mwananchi kuwa _____ (i) wa mazingira. Tukishirikiana, tutaweza kujenga mazingira _____ (j) kwa kizazi cha sasa na kijacho.

KAZI YA 3: SARUFI NA MSAMIATI Alama 30

3. Taja aina ya neno lililopigiwa mstari katika kila sentensi.

a) **Wanafunzi** walifanya utafiti kuhusu teknolojia. **(1 alama)**

_____

_____

_____

_____

c) Wakulima walipanda mazao **mengi** msimu huu. **(1 alama)**

_____

_____

d) Vijana **walishirikiana** katika mradi huo. **(1 alama)**

_____

_____

e) Mti **ule** ulikuwa mrefu sana. **(1 alama)**

_____

_____

f) Wanafunzi walifanya kazi **kwa bidii**. **(1 alama)**

_____

_____

4. Andika sentensi zifuatazo katika **wingi** bila kubadilisha maana.

a) Kitabu hiki kimepotea. **(2 alama)**

_____

_____

b) Mti huu umeanguka. **(2 alama)**

_____

_____

c) Jembe lile limevunjika. **(2 alama)**

_____

_____

5. Badilisha vitenzi vilivyopigiwa mstari kulingana na maagizo.

_____

_____

b) Mkulima **alipanda** miti mingi.

Badilisha kuwa **wakati ujao**. **(2 alama)**

_____

_____

c) Vijana **watashiriki** katika kampeni ya mazingira.

Badilisha kuwa **wakati uliopo**. **(2 alama)**

_____

_____

6. Andika sentensi zifuatazo katika hali ya **ukanushaji**.

a) Wanafunzi wamefanya usafi wa mazingira. **(2 alama)**

_____

_____

b) Mkulima atapanda miti kesho. **(2 alama)**

_____

_____

7. Andika kitenzi kilichomo kwenye mabano katika kauli uliyopewa.

a) Mama alim_____ mtoto chakula.

(–lish–)

Kauli ya kutendea (2 alama)

b) Wanafunzi wal_____ taarifa muhimu.

(–andik–)

Kauli ya kutendwa (2 alama)

8. Toa neno lenye maana sawa na lile lililopigiwa mstari.

a) Tabia hii imeleta **kero** kubwa katika jamii. **(1 alama)**

b) Wanafunzi wanapaswa kuwa **waangalifu** wanapotumia mtandao. **(1 alama)**

_____

_____

c) Jamii inapaswa **kuhifadhi** mazingira. **(1 alama)**

_____

_____

d) Taarifa hiyo ilikuwa **ya kweli**. **(1 alama)**

_____

_____

SEHEMU B: ALAMA 30

KAZI YA 4: UFAHAMU Alama 10

9. Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali yanayofuata.

UMUHIMU WA MIMEA NA WANYAMA

Mimea na wanyama ni sehemu muhimu ya mfumo wa mazingira. Mimea hutupatia oksijeni, chakula, dawa na malighafi zinazotumiwa katika viwanda mbalimbali. Miti pia husaidia kuhifadhi udongo na maji. Misitu inapohifadhiwa vizuri, huwa makazi ya viumbe wengi na huchangia katika kudhibiti mabadiliko ya tabianchi.

Wanyama nao wana umuhimu mkubwa katika mazingira na maisha ya binadamu. Baadhi yao hutupatia chakula, ngozi na bidhaa nyingine. Wanyama wa porini huvutia watalii na hivyo kuchangia mapato ya taifa. Aidha, wanyama mbalimbali hushiriki katika usawazishaji wa mfumo wa ikolojia.

Hata hivyo, shughuli za binadamu kama ukataji wa miti, uwindaji haramu, uchafuzi wa mazingira na upanuzi wa makazi zimeathiri mimea na wanyama. Baadhi ya viumbe viko katika hatari ya kutoweka. Ili kukabiliana na hali hii, jamii inapaswa kushirikiana na serikali katika kuhifadhi misitu, kulinda wanyamapori na kutumia maliasili kwa njia endelevu.

Maswali

a) Taja manufaa mawili ya mimea kwa binadamu. **(2 alama)**

_____

_____

b) Eleza namna wanyama wa porini wanavyosaidia uchumi wa taifa. **(2 alama)**

_____

_____

c) Taja shughuli mbili za binadamu zinazohatarisha mimea na wanyama. **(2 alama)**

_____

_____

d) Eleza maana ya kutumia maliasili kwa njia **endelevu**. **(2 alama)**

_____

_____

e) Pendekeza hatua mbili ambazo jamii inaweza kuchukua ili kuhifadhi mimea na wanyama. **(2 alama)**

_____

_____

KAZI YA 5: INSHA Alama 20

10. **Jibu swali moja pekee.**

A.

Anza insha yako kwa sentensi ifuatayo na uendeleze hadithi kwa mtiririko mzuri:

“Nilipofika shuleni asubuhi hiyo, niligundua kuwa kulikuwa na jambo lisilo la kawaida...”

Andika insha ya **maneno 250–300**.

(20 alama)

AU

B.

Endeleza insha kwa kutumia sentensi hizi kama mwanzo:

“Teknolojia inaweza kubadilisha maisha ya kijana kwa njia nyingi. Hata hivyo, matumizi yake yanahitaji

Insha yako iwe ya **maneno 250–300**.

(20 alama)

For more resources, visit cbckenyahub.com for marking schemes | 0712468452

For more resources, visit cbckenyahub.com for marking schemes | 0712468452

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA